JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO

# BAJETI YA SERIKALI YA MWAKA WA FEDHA 2019/20 KWA LUGHA RAHISI

## Toleo la Wananchi



Imetolewa na Wizara ya Fedha na Mipango
kwa kushirikiana na Policy Forum

# 1. UTANGULIZI

## 1.1 Bajeti Toleo la Wananchi

*Bajeti Toleo la Wananchi* hutolewa kila mwaka wa fedha tangu mwaka 2010/11 ili kumuwezesha mwananchi kuelewa bajeti ya serikali kwa urahisi. Ni toleo linaloielezea bajeti kwa wananchi katika uhalisia wake. Linatoa muhtasari wa rasilimali fedha ambazo serikali inatarajia kuzipata na zitakavyotumika kuleta maendeleo ya wananchi. *Toleo la Wananchi* 2019/20 linaanza na utangulizi unaojumuisha mchakakato wa bajeti kwa mwaka 2019/20. Toleo pia linaelezea kwa ufupi vipaumbele vya bajeti, mikakati na hatua muhimu zitalizochukuliwa kuiwezesha bajeti kuleta matokeo yaliyokusudiwa na jinsi fedha zitakavyotumika.

## 1.2 Mchakato wa Bajeti ya Mwaka 2019/20

Bajeti ya mwaka wa fedha 2019/20 imeandaliwa kwa kufuata *Mwongozo wa Mpango na Bajeti* uliotoa maelekezo na kubaini vipaumbele vya bajeti kwa mwaka 2019/20. Baada ya kuandaliwa bajeti iliwasilishwa katika ngazi tofauti kwa ajili ya kuidhinishwa ikiwemo baraza la mawaziri na kisha bungeni. Uwasilishaji wa bajeti bungeni ni kwa kuzingatia matakwa ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 na Sheria ya Bajeti ya mwaka 2015. Baada ya maandalizi na uidhinishwaji, hatua zinazofuata ni utekelezaji na ufuatiliaji wa bajeti ambapo wananchi na wadau wote kwa ujumla wanategemewa kushiriki kikamilifu katika hatua hizi.

# 2. VIPAUMBELE VYA BAJETI YA MWAKA 2019/20

Bajeti hii imelenga kuwainua wananchi kiuchumi na kuboresha mazingira ya kufanya biashara na kuwekeza hapa nchini. Dhima kuu ya bajeti hii itaendelea kuwa "**Kujenga Uchumi wa Viwanda Utakaochochea Ajira na Ustawi Endelevu wa Jamii**. Maeneo ya vipaumbele katika utekelezaji wa bajeti ni kama ifuatavyo:

### 2.1 Viwanda na Kilimo:

i. Kuvutia uwekezaji kwenye viwanda vinavyotumia malighafi zinazopatikana nchini kama vile mazao ya kilimo, mifugo, uvuvi, misitu na madini.
ii. Kuzalisha bidhaa kwa ajili ya soko la ndani na ziada kuuza nje ya nchi.
iii. Kuongeza fursa za ajira.
iv. Kutekeleza programu ya kuendeleza Sekta ya Kilimo hususan upatikanaji wa mbegu bora, pembejeo, huduma za ugani, masoko, miundombinu wezeshi na tafiti.
v. Kupeleka fedha kwenye maeneo wezeshi ya kilimo na kutoa unafuu wa kodi.
vi. Kuimarisha bodi za mazao, kuboresha na kuhamasisha uanzishaji wa vyama vya Ushirika vya mazao ili kupata mikopo kutoka kwenye taasisi za fedha kwa ajili ya kuwezesha shughuli za Kilimo.
vii. Kuanzisha viwanda vidogo vidogo vya kuongeza thamani ya mazao.

### 2.2 Ukuaji wa uchumi na maendeleo ya watu:

Kuimarisha upatikanaji wa huduma bora za afya, elimu na ujuzi, chakula na lishe bora, huduma za maji safi na salama pamoja na kuweka msukumo katika kuongeza ubora wa nguvu kazi ili iendane na mahitaji ya soko la ajira.


### 2.3 Uboreshaji wa mazingira ya uendeshaji biashara na uwekezaji:

Bajeti imeweka msukumo katika kuboresha mazingira ya biashara ili yawe rafiki na yenye gharama nafuu katika:

i. Kuendeleza ujenzi na ukarabati wa miundombinu hususan reli, bandari, nishati, barabara, madaraja na viwanja vya ndege.
ii. Kupitia na kuimarisha mifumo ya kisera, kisheria na kitaasisi.
iii. Kuimarisha ulinzi na usalama ili kushawishi na kuvutia wawekezaji wa ndani na nje.

### 2.4 Ufuatiliaji na Tathmini:

Bajeti inalenga kuimarisha ufuatiliaji na tathmini katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika ngazi zote. Vilevile, itaimarisha usimamizi wa ukusanyaji mapato ya kodi na yasiyo ya kodi bila kuathiri biashara.




## 3. SERA NA HATUA MUHIMU ZA KUIWEZESHA BAJETI

### 3.1 Matarajio Katika Ukuaji wa Uchumi kwa Mwaka wa Fedha 2019/20

Bajeti inalenga kukuza uchumi jumla kwa viwango vifuatavyo:

i. Pato la Taifa kukua kwa asilimia 7.1 mwaka 2019 kutoka ukuaji wa asilimia 7.0 mwaka 2018;
ii. Kudhibiti mfumuko wa bei kuendelea kubaki katika wigo wa tarakimu moja (kati ya asilimia 3.0 hadi 4.5);
iii. Mapato ya ndani kufikia asilimia 15.8 ya Pato la Taifa kwa mwaka wa fedha 2019/20 kutoka asilimia 14.3 mwaka 2018/19;
iv. Mapato ya kodi kufikia asilimia 13.1 ya Pato la Taifa kwa mwaka wa fedha 2019/20 kutoka matarajio ya asilimia 12.1 kwa mwaka 2018/19; na
v. Nakisi[1] ya bajeti kufikia asilimia 2.3 ya Pato la Taifa kwa mwaka wa fedha 2019/20.

### 3.2 Sera na Mikakati ya Kuongeza Mapato ya ndani kwa mwaka wa Fedha 2019/20

Ukusanyaji wa mapato ya ndani utaongezwa na kuimarishwa ili ugharamiaji wa shughuli za Serikali ikiwemo miradi mikubwa ya miundombinu na huduma za jamii. Katika kufanikisha azma hii, sera zifuatazo zitatekelezwa:


i. Kuboresha mazingira ya kufanya biashara ili kuvutia uwekezaji, ukuaji wa biashara ndogo na za kati ili kupanua wigo wa kodi na mapato mengine ya Serikali;
ii. Kurekebisha viwango vya kodi kwa lengo la kuhamasisha uzalishaji na kulinda viwanda vya ndani dhidi ya ushindani kutoka nje;
iii. Kujenga utamaduni wa ulipaji kodi kwa hiari, upanuzi wa wigo wa kodi na matumizi ya TEHAMA katika usimamizi wa kodi;
iv. Kuimarisha usimamizi wa sheria za kodi ili kutatua changamoto za ukwepaji kodi na kupunguza upotevu wa mapato, pamoja na kuweka mkazo utoaji wa elimu kwa mlipakodi;
v. Kuendelea kuwianisha na kupunguza tozo na ada mbalimbali zinazotozwa na Wakala, Taasisi na Mamlaka za Serikali za Mitaa; na
vi. Kuiongezea Mamlaka ya Mapato ya Tanzania uwezo hususan watumishi, vitendea kazi bora na mafunzo ili kutambua na kudhibiti mbinu za ukwepaji kodi.

Katika kufikia malengo ya makadirio ya mapato ya ndani, mikakati ifuatayo ya kiutawala itatekelezwa:

i. Kuongeza ufanisi katika usimamizi na ukusanyaji wa kodi za ndani kwa kutekeleza Mfumo Jumuishi wa Usimamizi wa Mapato ya Ndani;
ii. Kupanua wigo wa kodi kupitia utambuzi na usajili wa walipakodi wapya pamoja na kuendelea na zoezi la urasimishaji wa sekta isiyo rasmi;
iii. Kuwekeza kwenye maeneo ambayo Serikali inaweza kupata mapato zaidi hususan katika uvuvi wa bahari kuu kwa kujenga bandari ya uvuvi na ununuzi wa meli za uvuvi;
iv. Kuimarisha uwezo wa ufuatiliaji na udhibiti wa uhamishaji wa faida unaofanywa na kampuni za kimataifa;
v. Kuimarisha usimamizi wa misamaha ya kodi kwa kuhakikisha inaelekezwa kwenye miradi inayokusudiwa;

[1] **Nakisi ya bajeti** ni pengo kati ya kiasi kinachotarajiwa na kinachopatikana katika kipindi husika.

vi. Kuhakikisha kuwa maduhuli yote yanapitia katika Mfumo wa Serikali wa Kielektroniki wa Ukusanyaji wa Mapato (GePG); na
vii. Kuimarisha mifumo ya ufuatiliaji katika taasisi za Serikali ili kuhakikisha kuwa michango stahiki ya Taasisi za Umma kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali inawasilishwa kwa wakati.




### 3.3 Sera na Hatua za Kusimamia Matumizi

Sera za matumizi katika bajeti ya mwaka wa fedha 2019/20 zinajumuisha:

i. Kuendelea kusimamia nidhamu katika matumizi ya fedha za umma;
ii. Kudhibiti nakisi ya bajeti isizidi asilimia 2.3 ya Pato la Taifa;
iii. Kuelekeza fedha kwenye maeneo ya kipaumbele na yenye kuchochea ukuaji wa uchumi; na
iv. Kuendelea kudhibiti kuongezeka kwa malimbikizo ya madeni kwa Serikali.

Katika kusimamia sera za matumizi, hatua zifuatazo zitachukuliwa:

i. Kuendelea kufanya ufuatiliaji na tathmini ya matumizi hususan katika miradi ya maendeleo ili zitumike kama ilivyokusudiwa;
ii. Kuendelea kulipa malimbikizo ya madeni ya Serikali yaliyohakikiwa;
iii. Maafisa Masuuli (waidhinishaji wa fedha) kutoingia mikataba bila kuwa na uhakika wa upatikanaji wa fedha au ridhaa ya Mlipaji Mkuu wa Serikali; na
iv. Hatua za kisheria, kiutawala na kinidhamu kwa watakaothibitika kwenda kinyume na sheria na kanuni zinazoongoza utendaji katika taasisi zao.

# 4. MABORESHO YA MIFUMO YA KODI, ADA NA TOZO MBALIMBALI

Katika mwaka wa fedha 2019/20, Serikali itaendelea kuwa na mfumo wa kodi ambao ni tulivu na wakutabirika kwa kufanya maboresho mbali mbali kwenye baadhi ya viwango vya kodi, tozo na ada zinazotozwa chini ya sheria na taratibu mbalimbali. Aidha, mabadiliko yanalenga kuchochea kasi ya ukuaji wa uchumi hususani katika sekta ya kilimo, viwanda, kukuza ajira, kuboresha biashara na kuongeza mapato. Baadhi ya maboresho hayo ni kama yafuatayo:

### 4.1 Marekebisho katika sheria ya Ongezeko la Thamani (VAT),

i. Kupunguza VAT hadi kuwa asilimia sifuri (0) kwenye huduma ya umeme unaouzwa kutoka Tanzania Bara kwenda Tanzania Visiwani ili kupunguza gharama za maisha kwa wananchi wa Tanzania Zanzibar;

ii. Kufanya marekebisho kuhusu uuzaji wa mazao ya kilimo nje ya nchi na kuwawezesha wauzaji wa mazao ghafi nje ya nchi kuendelea kufanya biashara kadri ya kibali kitakavyotolewa na Serikali;

iii. Kusamahe Kodi ya VAT kwenye:

- Makasha yenye majokofu yanayotumika kwenye kilimo cha kisasa cha mbogamboga kwa wakulima watakaoingiza makasha hayo kutoka nje ya nchi kwa matumizi ya kilimo, ili kupunguza gharama za uzalishaji na kuhamasisha kilimo cha kisasa cha mboga mboga;
- Vifaa vya kukaushia nafaka ili kutoa nafuu kwenye gharama za kukausha nafaka kwa ajili ya kuzihifadhi ili kuchochea ukuaji wa kilimo cha mazao ya nafaka;
- Vilainishi vya ndege vinavyoingizwa nchini na waendeshaji wa ndani, Shirika la Ndege la Taifa, au mashirika ya ndege yanayotambulika katika Mikataba ya Kimataifa ya Huduma za Anga. Hatua hii itawezesha nchi yetu kusaini Mikataba ya Kimataifa ya Huduma za Anga iliyoshindikana kusaininiwa awali kutokana na kutokuwepo kwa msamaha huo;

### 4.2 Marekebisho katika sheria ya Kodi ya Mapato, kwa:

i. Kupunguza kiwango cha Kodi ya Mapato ya Makampuni kutoka asilimia 30 mpaka asilimia 25 kwa miaka miwili kuanzia mwaka wa fedha 2019/20 kwa wawekezaji wapya wa viwanda vya kuzalisha taulo za kike ili kuvutia uwekezaji katika kuzalisha bidhaa hiyo muhimu ndani ya nchi;

ii. Kutoa msamaha wa kutengeza hesabu ambazo zinatakiwa kuwasilishwa TRA kwa ajili ya kukokotoa Kodi ya Mapato kutoka kiwango cha sasa cha milioni ishirini mpaka shilingi milioni mia moja ili kupunguza gharama za mlipa kodi kwa ajili ya mtaalam wa kutengezeza hesabu na kuchochea ulipaji kodi wa hiari;

iii. Kutoa msamaha katika:

- Kodi ya Zuio inayotozwa kwenye gharama zinazoambatana na mikopo inayotolewa na Benki, Taasisi za Fedha za nje na wahisani mbalimbali kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya Serikali ili kuiwezesha Serikali kutekeleza miradi yake kwa wakati;
- Kodi kwenye mauzo ghafi yasiyozidi shilingi milioni nne kwa wenye vitambulisho vya wajasiriamali na kupunguza kiwango cha chini cha kodi kutoka shilingi laki moja na nusu mpaka shilingi laki moja kwa mwaka ili kupunguza mzigo wa kodi kwa walipa kodi wadogo.

### 4.3 Marekebisho katika Sheria ya Ushuru wa Bidhaa kwa:

i. Kutokufanya mabadiliko ya viwango maalum vya Ushuru wa Bidhaa kwa bidhaa zote zisizo na petroli;
ii. Kutoza Ushuru wa Bidhaa wa asilimia 10 kwenye nywele za bandia zinazotengenezwa ndani ya nchi na asilimia 25 kwenye nywele kutoka nje ya nchi;
iii. Kutoza Ushuru wa Bidhaa wa asilimia 10 kwenye bidhaa za mabomba na vifaa vya plastiki vinavyotumika kwenye ujenzi wa miundombinu ya maji ili kulinda viwanda vya ndani na kuongeza fursa za kazi, ajira na mapato ya Serikali;
iv. Kupunguza ushuru wa Bidhaa kwenye mvinyo uliotengenezwa kutokana na usindikaji wa matunda yanayozalishwa hapa nchini tofauti na zabibu kutoka shilingi 200 kwa lita hadi shilingi 61 ili kuvutia uwekezaji kwenye viwanda vidogo vidogo vya aina hii nchini na kuhamasisha ulipaji kodi wa hiari;

### 4.4 Marekebisho ya Sheria ya Usimamizi wa Kodi

Kuongeza muda wa ziada wa miezi sita mpaka Disemba 2019 kwa walipa kodi waliokubaliwa kulipa kodi wanazodaiwa kwa utaratibu maalum wa kusamehe malimbikizo ya nyuma ya riba ili kutoa ahueni kwa walipakodi waliokuwa na malimbikizo makubwa yanayoathiri biashara zao.

### 4.5 Marekabisho ya Sheria ya Usalama Barabarani

i. Kuongeza muda wa leseni za udereva kutoka miaka mitatu ya sasa mpaka miaka mitano;
ii. Kuongeza tozo ya leseni ya udereva kutoka shilingi elfu arobaini na kufikia elfu sabini;
iii. Kuongeza ada ya kadi ya usajili wa magari kutoka shilingi 10,000 hadi shilingi 50,000; Pikipiki za matairi matatu kutoka shilingi 10,000 hadi shilingi 30,000; Pikipiki kutoka shilingi 10,000 hadi shilingi 20,000.

### 4.6 Marekebisho madogo madogo katika baadhi ya Sheria za Kodi na Sheria nyingine mbalimbali.

Katika hatua ya utekelezaji wa Mpango Kazi wa **Kuboresha Mfumo wa Udhibiti wa Biashara**, ada na tozo zipatazo 54 zimefutwa ili kuondoa muingiliano wa majukumu ya kiutendaji baina ya Wizara, taasisi na Mamlaka za Udhibiti. Marekebisho hayo yamejumuisha ***Mamlaka ya Dawa (TFDA), Shirika la Viwango Tanzania, Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali, Sheria ya Usimamizi na Udhibit wa Kemikali za Majumbani na Viwandani, Wizara ya Mifugo na Uvuvi- Sekta ya Mifugo, Wizara ya Maliasili na Utalii*** na ***Wizara ya Maji***.

### 4.7 Marekebisho yamefanyika pia kwenye Sheria ya Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya Mwaka 2004

Kwa ajili ya kuendeleza viwanda, kukuza ajira na kuboresha maisha ya wananchi katika nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.


# 5. NAMNA SERIKALI INAVYOTARAJIA KUPATA MAPATO

Katika Mwaka 2019/20, Serikali imepanga kukusanya kiasi cha shilingi **bilioni 33,105.4** Mchanganuo wa makusanyo haya ni kama ifuatavyo:

i. **Mapato ya ndani** yenye jumla ya **shilingi bilioni 23,045.3** yakijumuisha mapato yatokanayo na kodi ya **Shilingi bilioni 19,100.9,** mapato yasiyo ya kodi ya **shilingi bilioni 3,178.9** pamoja na mapato ya ndani ya Mamlaka za Serikali za Mitaa ya **Shilingi bilioni 765.4.**

ii. **Misaada na mikopo nafuu** yenye jumla ya **shilingi bilioni 2,783.7** ikijumuisha **Shilingi bilioni 272.8** ikiwa ni misaada na mikopo nafuu ya kibajeti, **Shilingi bilioni 2,311.4** ikiwa ni misaada na mikopo nafuu ya miradi ya Maendeleo, pamoja na **Shilingi bilioni 199.5** kwa ajili ya misaada na mikopo nafuu ya kisekta.

iii. **Mikopo ya ndani na nje yenye masharti ya kibiashara** yenye jumla ya **Shilingi bilioni 7,276.4** ikijumuisha; **Shilingi bilioni 2,316.4** mikopo ya nje, na **Shilingi bilioni 4,960.0** - mikopo ya ndani.




# 6. SERIKALI INAVYOTARAJIA KUTUMIA MAPATO

## 6.1 Matumizi ya Mwaka wa Fedha 2019/20 katika maeneo makuu ya Kibajeti

Mwaka wa fedha 2019/20, Serikali imepanga kutumia jumla ya **shilingi bilioni 33,105.4** kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo. Kati ya fedha hizo:


i. **Shilingi bilioni 20,856.8** zimetengwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida ikiwa ni asilimia 63 ya bajeti, ikijumuisha **shilingi bilioni 9,721.1** kwa ajili ya ulipaji wa deni la Serikali (*malipo ya riba, mtaji, michango ya Serikali kwenye Mifuko ya Hifadhi ya Jamii na matumizi mengine ya mfuko*) na **shilingi bilioni 7,558.9** kwa ajili ya mishahara. Aidha, **shilingi bilioni 3,576.7** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo ikijumuisha **shilingi bilioni 2,956.1** kwa ajili ya uendeshaji wa ofisi za Serikali, **shilingi bilioni 160.0** kwa ajili kulipa madeni yaliyohakikiwa pamoja na **shilingi bilioni 460.5** kwa ajili ya matumizi yatokanayo na vyanzo vya ndani vya Halmashauri.

ii. Matumizi ya maendeleo yanatarajiwa kuwa **shilingi bilioni 12,248.6** sawa na asilimia 37 ya bajeti yote, ambapo kiasi cha **Shilingi bilioni 9,737.7** ni fedha za ndani na **shilingi bilioni 2,510.8** ni fedha za nje. Kati ya fedha za maendeleo za ndani zilizotengwa, **shilingi bilioni 8,992.8** ni kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo ikijumuisha ujenzi wa reli ya kisasa kwa kiwango cha *Standard Gauge*; mradi wa kufua umeme Mto Rufiji; Mifuko ya Reli, Maji na Umeme vijijini; kugharamia mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu; kugharamia elimu msingi bila ada.



iii. **Ruzuku kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa:** Kwa mwaka wa fedha 2019/20, ruzuku ya jumla ya **shilingi bilioni 5,482.3** itapelekwa kwenye Mamlaka ya Serikali za Mitaa. Kati ya fedha hizo **shilingi bilioni 4,320.3** ni matumizi ya kawaida ambapo **shilingi bilioni 3,669.3** ni mishahara na **shilingi bilioni 650.9** ni matumizi mengineyo. Ruzuku ya fedha za maendeleo inatarajiwa kuwa **shilingi bilioni 1,162.0** ikijumuisha **shilingi bilioni 797.4** fedha za Ndani na **shilingi bilioni 364.6** fedha za nje. Mchanganuo wa ruzuku kisekta kwenye Serikali za Mitaa ni kama ufuatavyo: -

- Sekta ya elimu shilingi bilioni **2,904.8**
- Sekta ya afya shilingi bilioni **835.3**
- Sekta ya kilimo shilingi bilioni **88.1**
- Sekta ya barabara shilingi bilioni **251.2**
- Sekta ya maji shilingi bilioni **19.7** na
- Sekta ya utawala shilingi bilioni **1,097.8**
- Ruzuku kwa ajili ya miradi ya kuongeza mapato katika Halmashauri shilingi bilioni **70.0**




## 6.2 Mipango ya Matumizi ya Mwaka wa Fedha 2019/20 kwa Sekta

Muhtasari wa mipango na matumizi ya mwaka 2019/20 kwenye programu, miradi na shughuli mbalimbali kwenye sekta kwa nchi nzima ni kama ifuatavyo:

## 6.2.1 Elimu



ya kutekeleza shughuli mbalimbali katika Sekta ya Elimu. Baadhi ya shughuli hizo ni pamoja na: kuendelea kutoa Elimu Msingi Bila Ada; kuendelea kugharamia Mitihani ya Taifa; kuendelea na utoaji wa mikopo kwa wanafunzi wa Elimu ya Juu na kutekeleza miradi ya maendeleo ya elimu kupita programu mbalimbali.

Baadhi ya matumizi kwenye sekta hii ni kama ifuatavyo:

i. **Shilingi bilioni 288.4** zimetengwa kugharamia Elimu Msingi Bila Ada katika bajeti za mikoa na halmashauri zote nchini;
ii. **Shilingi bilioni 165.62** kwa ajili ya miradi ya kuboresha miundombinu ya elimu ya Msingi na Sekondari kupitia programu mbalimbali;
iii. **Shilingi bilioni 73.97** kwa ajili ya uendeshaji wa mitihani ya kitaifa ya shule za msingi, sekondari na vyuo vya ualimu nchi nzima;
iv. Shilingi bilioni **162.94** zimeelekezwa katika vyuo vikuu na vyuo vya ufundi stadi nchini ili kuboresha miundombinu na kuimarisha huduma zinazotolewa na vyuo hivyo; **Shilingi bilioni 450.00** zitatumika kutoa mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu;
v. **Shilingi bilioni 75.35** kwa ajili ya kugharamia masuala ya utafiti, sayansi, teknolojia na ubunifu; na
vi. **Shilingi bilioni 218.38** kwa ajili ya usimamizi na ufuatiliaji wa masuala ya elimu kupitia taasisi, idara na vitengo vinavyosimamia masuala ya elimu nchini.

## 6.2.2 Afya



Bajeti ya Sekta ya Afya kwa mwaka wa fedha 2019/20 ni **shilingi bilioni 1,822.5**. Baadhi ya shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni pamoja na: Kuendelea kuimarisha na kuboresha utoaji wa huduma za chanjo; kuimarisha upatikanaji wa dawa, vifaa, vifaa tiba, vitendanishi katika vituo vya umma vya kutolea huduma za afya; Kuendelea kuboresha huduma za Afya ya uzazi, mama na mtoto; Kuboresha miundombinu na utoaji huduma katika Hospitali za Rufaa za mikoa; Kuimarisha huduma za kibingwa katika Hospitali za Taifa, Maalum na Kanda nchini; na Kuimarisha mifumo ya utoaji taarifa pamoja na ile ya Kielekitroniki katika Hospitali za Rufaa za Mikoa. Katika kutekeleza vipaumbele hivyo, fedha zimetengwa kwa ajili ya kufanya shughuli mahsusi zifuatazo:

i. **Shilingi bilioni 30.0** kwa ajili ya ununuzi na usambazaji wa Chanjo;
ii. **Shilingi bilioni 200.0** kwa ajili ya ununuzi wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi;
iii. **Shilingi bilioni 4.3** kwa ajili ya ujenzi wa vituo 12 vya damu salama katika Mikoa 12 ya Dar Es Salaam, Mwanza, Morogoro, Geita, Kigoma, Mtwara, Mbeya, Tabora, Dodoma, Pwani, Arusha na Kagera;
iv. **Shilingi Bilioni 2.0** kwa ajili ya kuimarisha uhamasishaji wa ukusanyaji wa damu salama pamoja na uhifadhi;
v. **Shilingi bilioni 4.0** kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa jengo la kutolea huduma za wagonjwa wanaojigharamia katika Hospitali ya Taifa Muhimbili;
vi. **Shilingi bilioni 1.0** kwa ajili ya kuimarisha huduma za kibingwa katika Taasisi ya Tiba ya Moyo Jakaya Kikwete;
vii. **Shilingi bilioni 5.0** kwa ajili ya kufanya upanuzi wa wodi za wazazi na kutenga vyumba vya wagonjwa Mahututi wanaotokana na uzazi katika hospitali za Rufaa za mikoa mitano;
viii. **Shilingi bilioni 12.0** kwa ajili ya kuendelea na Ujenzi wa Hospitali za Rufaa nchini;
ix. **Shilingi bilioni 10.0** kwa ajili ya kuboresha utoaji huduma katika Taasisi ya Cancer ya Ocean Road;
x. **Shilingi bilioni 5.0** kwa ajili ya kuboresha utoaji huduma katika Taasisi ya Mifupa MOI;
xi. **Shilingi bilioni 1.9** kwa ajili ya kuboresha utoaji huduma katika Hospitali ya Kibong`oto; na
xii. **Shilingi bilioni 1.7** kwa ajili ya kuboresha utoaji huduma katika Hospitali ya Bugando.

## 6.2.3 Maendeleo ya Uchumi

Sekta hii imetengewa jumla ya Shilingi bilioni 8,687.5 ili kuhudumia sekta ndogo za Kazi Usafirishaji na Mawasiliano, Kilimo, Viwanda, Biashara, Nishati, Madini, Maliasili, Utalii na Mazingira, Vijana, Ajira na Undelezaji wa Ujuzi

### Ujenzi, Usafirishaji na Mawasiliano



ustawi endelevu wa jamii, Serikali imeendelea kuweka msisitizo mkubwa katika kuendeleza na kuimarisha ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya kiuchumi hususani barabara na madaraja, reli, bandari, na viwanja vya ndege. Ili kufanikisha azma hii, katika bajeti ya mwaka wa fedha 2019/20, Serikali imetenga jumla ya **shilingi bilioni 5,519.5** kwa sekta ya Ujenzi, Usafirishaji na Mawasiliano. Baadhi ya matumizi kwenye sekta hizi ni pamoja na:

i. **Shilingi bilioni 2,476.1** kwa ajili ya ujenzi wa reli mpya ya kati kwa kiwango cha *Standard Gauge;*
ii. **Shilingi bilioni 1,046.7** kwa ajili ya matengezo ya barabara kuu, barabara za mikoa, madaraja na uendeshaji wa mizani nchini;
iii. **Shilingi bilioni 500.0** kwa ajili ya ununuzi wa ndege aina ya Boeing 787 Dreamliner na Bombadier Q400 pamoja na gharama za matengenezo;
iv. **Shilingi bilioni 216.0** kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya reli ya kati kutoka Dar-es Salaam hadi Isaka;
v. **Shilingi bilioni 255.7** kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya reli kupitia Mfuko wa Reli;
vi. **Shilingi bilioni 102.2** kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya viwanja vya ndege nchini;
vii. **Shilingi bilioni 70.0** kwa ajili ya ujenzi wa meli mpya na ukarabati wa meli zilizopo katika Ziwa Victoria na Tanganyika;
viii. **Shilingi bilioni 53.1** kwa ajili ya ununuzi, ujenzi na ukarabati wa vivuko pamoja na upanuzi wa maegesho ya vivuko katika maeneo mbalimbali nchini;
ix. **Shilingi bilioni 11** kwa ajili ya Ujenzi wa Daraja jipya la Selander; na
x. **Shilingi bilioni 251.7** kwa ajili ya matengenezo ya barabara za mijini na vijijini kupitia Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (*TARURA*).

### Kilimo



Kilimo kinajumuisha mazao, umwagiliaji, mifugo, uvuvi, ushirika, misitu na nyuki. Kilimo kinachangia asilimia 30.1 ya pato la Taifa, inatoa ajira kwa Watanzania kwa asilimia 65.5 na inachangia asilimia 65 ya malighafi za viwanda.

Katika mwaka 2019/20, serikali imetenga **shilingi bilioni 543.9** kwa ajili ya kutekeleza malengo ya kimkakati yatakayohakikisha usalama wa chakula na upatikanaji wa malighafi kwa ajili ya viwanda. Maeneo ya kipaumbele na matumizi yake ni kama ifuatavyo:

i. **Shilingi bilioni 29.6** zimetengwa kwa ajili ya kuboresha upatikanaji wa pembejeo za kilimo, uzalishaji wa mbegu bora za mazao, udhibiti wa visumbufu, matumizi ya zana bora za kilimo na huduma za ugani;
ii. **Shilingi bilioni 32.5** kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya umwagiliaji;
iii. **Shilingi bilioni 75.7** kwa ajili Ujenzi wa maghala, masoko na miundombinu ya kuhifadhi mazao ya kilimo;
iv. **Shilingi bilioni 36.6** kwa ajili ya kuimarisha utafiti na mafunzo ya kilimo;
v. **Shilingi bilioni 11.4** kwa ajili ya kusimika mfumo endelevu wa upatikanaji na usambazaji wa pembejeo na zana za kilimo nchini;
vi. **Shilingi bilioni 5.5** kwa ajili ya kusajili, kuandaa kanzidata ya wakulima na kuanzisha utaratibu wa bima ya mazao zimetengwa;
vii. **Shilingi bilioni 3.0** kwa ajili ya kuhamasisha uwekezaji kwenye ufugaji wa kibiashara
viii. **Shilingi bilioni 1.0** kwa ajili ya kuimarisha miundombinu ya uvuvi;
ix. **Shilingi billion 14.7** kwa ajili ya udhibiti na matumizi endelevu ya rasilimali za uvuvi;
x. **Shilingi bilioni 8.0** kwa ajili ya kuimarisha Ushirika.

## Viwanda na Biashara



Katika mwaka wa Fedha 2019/20 Viwanda na Biashara imetengewa jumla ya shilingi **bilioni 287.9**. Bajeti hii imelenga kufanya tathmini ya hali halisi ya uzalishaji na mahitaji ya bidhaa viwandani; Kufuatilia na kusimamia miradi ya kimkakati kama vile Liganga na Mchuchuma; Kufanya tathmini ya utekelezaji wa mikakati ya pamba hadi mavazi, alizeti na ngozi; Kuhamasisha uendelezaji wa sekta ya mafuta ya mawese; Kuwezesha upatikanaji wa mtaji kwa wajasiriamali wadogo na wa kati; Kuendeleza majadiliano ya kibiashara kati ya Nchi na Nchi, Kikanda na Kimataifa kwa ajili ya kupanua fursa za masoko na uwekezaji ili kuvutia uwekezaji nchini. Bajeti hii imelenga kutekeleza miradi mbalimbali ikiwemo:

i. **Shilingi bilioni 1.16** kwa ajili ya kugharamia Mradi wa Makaa ya Mawe Mchuchuma na Liganga (Njombe);
ii. **Shilingi bilioni 9.0** kwa ajili ya Mradi wa Maeneo Maalum ya Kiuchumi (SEZ) yaliyotengwa ikiwemo *Bagamoyo Technology Park*, William Benjamin Mkapa pamoja na *Kurasini Trade and Logistic centre;*
iii. **Shilingi billion 1.5** kwa ajili ya Kiwanda cha Matairi Arusha;
iv. **Shilingi bilioni 1.0** kwa ajili ya Mradi wa UNIDO – Programu Jumuishi ya Maendeleo ya Viwanda;
v. **Shilingi bilioni 5.0** kwa ajili ya Mradi wa Magadi Soda - Ziwa Natron na Engaruka;
vi. **Shilingi bilioni 8.0** kwa ajili ya kuendeleza tafiti za maendeleo ya viwanda katika Taasisi za *TIRDO, TEMDO* na *CAMARTEC*;
vii. **Shilingi bilioni 5.0** kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya viwanda vidogo (SIDO) katika mikoa ya Tabora, Kigoma, Iringa, Lindi, Morogoro, Mtwara, Mwanza na Kagera;
viii. **Shilingi bilioni 1.0** kwa ajili ya Mfuko wa Wajasiriamali (*NEDF-SIDO*) ili kuongeza mtaji wa kukopesha na kuweza kutoa mikopo ya mashine na mtaji wa viwanda vidogo.
ix. **Shilingi bilioni 7.5** kwa ajili ya Mradi wa Matrekta ya *URSUS TAMCO* pamoja na kuendeleza Eneo la Viwanda (*TAMCO*) – Kibaha;
x. **Shilingi bilioni 4.64** kwa ajili ya miradi mbali mbali ikiwemo NDC, TANTRADE, COSOTA, Kuanzisha na kuendeleza mfumo wa stakabadhi za Ghala katika mazao ya Chai, Kokoa, Kahawa, Ufuta na Dengu;

## Nishati



ajili ya kutekeleza vipaumbele mbalimbali ikiwa ni kuongeza uzalishaji wa umeme nchini ili kufikia lengo la kuwa na *MW 10,000* ifikapo mwaka 2025, pamoja na kutekeleza awamu ya tatu ya mradi wa umeme vijijini kupitia wakala wa nishati vjijini katika vijiji 1,990 vilivyosalia.

Baadhi ya matumizi kwenye sekta hii ni kama ifuatavyo: -

i. **Shilingi bilioni 1,443.0** kwa ajili ya Mradi wa kuzalisha umeme kwa kutumia maji ya mto Rufiji MW 2,115;

ii. **Shilingi bilioni 423.10** kwa ajili ya mradi wa kusambaza umeme vijijini;

iii. **Shilingi bilioni 60.0** kwa ajili ya mradi wa kuzalisha umeme kwa kutumia gesi asilia wa Kinyerezi MW 185;

iv. **Shilingi bilioni 12.5** kwa ajili ya mradi wa kuzalisha umeme kwa kutumia maji wa Ruhuji MW 358;

v. **Shilingi bilioni 11.22 kwa ajili ya kutekeleza mradi wa kusambaza gesi asilia viwandani;**

vi. **Shilingi bilioni 11** kwa ajili ya mradi wa njia ya kusafirisha umeme Msongo wa KV 400 Rufiji, Chalinze, Dodoma;

vii. **Shilingi bilioni 7.0** kwa ajili ya mradi wa bomba la kusafirisha mafuta ghafi la Afrika Mashariki kutoka Uganda hadi bandari ya Tanga Tanzania;

viii. **Shilingi bilioni 4.0** kwa ajili ya mradi wa njia ya kusafirisha umeme wa msongo wa KV 400 wa Singida, Arusha Namanga;

ix. **Shilingi bilioni 3.0** kwa ajili ya mradi kuzalisha umeme kwa kutumia maji wa Rusumo MW80; na

x. **Shilingi bilioni 0.8** kwa ajili ya kutekeleza kazi za awali za mradi wa kusafirisha gesi asilia kutoka Tanzania kwenda Uganda.

## Madini




madini. Maeneo ya kipaumbele ni pamoja na: kuendeleza uchimbaji mdogo na wa kati wa madini; kuhamasisha shughuli za uongezaji thamani madini; kuimarisha ufuatiliaji na ukaguzi wa usalama, mazingira na uzalishaji wa madini katika migodi midogo, ya kati na mikubwa; kuboresha mazingira ya kuwawezesha Wananchi kunufaika na rasilimali za madini; kuendelea na uanzishwaji na usimamizi wa masoko ya madini; kudhibiti utoroshwaji wa madini katika maeneo yote nchini. Baadhi ya matumizi kwenye sekta hii ni kama ifuatavyo:

i. Shilingi **bilioni 6.0** kwa ajili ya Usimamizi Endelevu wa Rasilimali za Madini; na
ii. Shilingi **bilioni 1.04** kwa ajili Uhamasishaji, Uwazi na Uwajibikaji katika Rasilimali Madini, Mafuta na Gesi Asilia- TEITI.

## Maliasili, Utalii na Mazingira



Katika mwaka wa fedha 2019/20 Serikali imetenga jumla ya **Shilingi billioni 111.3** kwa ajili ya kuhifadhi na kusimamia matumizi endelevu ya maliasili na malikale, mazingira pamoja na kuchochea maendeleo ya utalii nchini. Baadhi ya matumizi ni pamoja na: -

i. Shilingi **billioni 14.6** kwa ajili ya usimamizi endelevu wa maliasili na malikale na kupambana na ujangili;

ii. Shilingi **billioni 13.3** kwa ajili ya usimamizi endelevu wa uhifadhi wa misitu na mazingira asilia na kuongeza thamani kwa mazao ya misitu;
iii. Shilingi **billioni 20.0** kwa ajili ya na kuendeleza utalii nchini;
iv. Shilingi **billioni 18.2** kwa ajili ya kuimarisha mifumo ya ikolojia ili kuhimili athari za mabadiliko ya tabianchi.

## Vijana, Ajira na Uendelezaji wa Ujuzi



Katika mwaka wa fedha 2019/20 jumla ya **Shilingi bilioni 32.7** zimetengwa kwa ajili ya kuweka mazingira wezeshi na uwezeshaji wananchi kiuchumi kupitia programu mbalimbali ili kuibua fursa na ukuzaji wa ajira pamoja na uendelezaji wa ujuzi. Matumizi katika sekta ndogo hii yatajumuisha:

i. **Shilingi bilioni 18.0** kwa ajili ya kutekeleza programu ya kukuza ujuzi nchini na kuongeza fursa za ajira na kazi zenye staha. Programu hii itahusisha:
   - ⇨ **Shilingi bilioni 3.6** kwa ajili ya kutoa mafunzo ya kilimo cha kisasa na ya kuongeza thamani ya bidhaa za mazao ya kilimo kwa vijana 20,000;
   - ⇨ **Shilingi bilioni 4.1** kwa ajili ya kutoa mafunzo kwa wanagenzi 3,000 kupitia kwa waajiri na taasisi za mafunzo;
   - ⇨ **Shilingi bilioni 1.4** kwa ajili ya **k**uwapatia ujuzi wa teknolojia mpya na mbinu za viwanda waajiriwa 450 wa sekta binafsi na kuwezesha wahitimu 500 kupata mafunzo mahala pa kazi;
   - ⇨ **Shilingi bilioni 0.2** kwa ajili ya kutoa mafunzo ya kilimo cha kisasa, ufugaji na uvuvi kwa watu 300 wenye ulemavu;
   - ⇨ **Shilingi bilioni 3.1** kwa ajili ya kurasimisha ujuzi wa watu 10,000 wa nje ya mfumo rasmi na
   - ⇨ **Shilingi bilioni 1.1** kwa ajili ya ununuzi wa vitendea kazi vya wanufaika wa Programu hii.

ii. **Shilingi bilioni 1.0** kwa ajili ya kutoa mikopo yenye masharti nafuu kwa vikundi vya vijana; na
iii. **Shilingi bilioni 2.9** kwa ajili ya kuwawezesha wananchi kiuchumi kwenye sekta binafsi.

## 6.2.4 Maji, Nyumba na Maendeleo ya Jamii

Sekta hii imetengewa jumla ya **shilingi 807.15** ikijumuisha sekta ndogo za Maji, Ardhi, Nyumba na Makazi pamoja na Maendeleo ya Jamii.

### Maji



Katika mwaka wa fedha 2019/20, Sekta ndogo ya Maji imetengewa shilingi bilioni 661.09 kwa ajili ya ujenzi, ukarabati na utekelezaji wa miradi ya maji mijini na vijijini ili kuhakikisha kuwa kunakuwa na rasilimali endelevu za majisafi na usafi wa mazingira. Vipaumbele vitakavyotekelezwa ni pamoja na: kuimarisha mifumo ya kukusanya takwimu za rasilimali za maji na tahadhari ya mafuriko nchini; kuzijengea uwezo Bodi za Maji za Mabonde. Baadhi ya matumizi kwenye sekta hii ni kama ifuatavyo:

i. Shilingi **bilioni 187.06** kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maji vijijini;
ii. **Shilingi bilioni 29.28** kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa Same - Mwanga – Korogwe;
iii. **Shilingi bilioni 10.3** kwa ajili ya mradi wa ujenzi na ukarabati wa mabwawa;
iv. **Shilingi bilioni 2.1** kwa ajili ya kuhamasisha matumizi ya nishati ya jua katika miradi ya maji vijijini;
v. **Shilingi bilioni 2.5** kwa ajili ya upembuzi yakinifu na usanifu wa mradi wa maji Ismani (Iringa Vijijini) na miradi ya maji pembezoni mwa Maziwa Makuu (Victoria, Nyasa na Tanganyika);
vi. **Shilingi bilioni 1.1** kwa ajili ya mradi wa Lukululu utakaohudumia vijiji 12 katika Wilaya ya Mbozi; na
vii. **Shilingi bilioni 2.04** kwa ajili ya miradi ya maji vijijini, Kigoma.



## Ardhi, Nyumba na Makazi





Katika mwaka wa fedha 2019/20 jumla ya shilingi bilioni 68.2 zimetenga kwa ajili ya sekta ndogo ya Ardhi, nyumba na makazi. Lengo ni kuimarisha huduma za miliki na urasimishaji wa ardhi katika ngazi za Mikoa na Halmashauri zote nchini, kuongeza mchango wa Sekta ya ardhi katika kukuza uchumi na kuhakikisha ardhi inatumika kwa tija na kuwa na makazi bora endelevu. Baadhi ya matumizi kwenye Sekta hii ni pamoja na:

i. **Shilingi bilioni 8.0** kwa ajili ya Mpango wa Ufuatiliaji na udhibiti wa Ardhi;
ii. **Shilingi bilioni 6.0** kwa ajili ya programu ya kuwezesha umilikishaji wa ardhi;
iii. **Shilingi bilioni 5.4** kwa ajili ya uimarishaji wa mipaka ya kimataifa;
iv. **Shilingi bilioni 3.4** kwa ajili ya mradi wa maendeleo ya ardhi na mipango miji;
v. **Shilingi bilioni 3.2** kwa ajili ya mradi wa uboreshaji wa umiliki wa ardhi;
vi. **Shilingi bilioni 2.6** kwa ajili ya mradi wa matumizi bora ya ardhi;
vii. **Shilingi bilioni 1.1** kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa nyumba za Serikali;
viii. **Shilingi bilioni 0.5** kwa ajili ya ukuzaji wa teknolojia ya ujenzi wa nyumba za bei nafuu;

## Maendeleo ya Jamii



Sekta ndogo ya Maendeleo ya Jamii imetengewa jumla ya shilingi bilioni 47.0 kwa ajili ya kuboresha utoaji huduma za ustawi na maendeleo ya jamii. Miongoni mwa maeneo ya vipaumbele na fedha zilizotengwa ni kama ifuatavyo:

i. **Shilingi bilioni 8.3** kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa miundombinu katika Taasisi za Maendeleo ya Jamii Tengeru, Vyuo vya Maendeleo ya Jamii, Taasisi ya Ustawi wa Jamii pamoja na Chuo cha Ustawi wa Jamii Kisangara;
ii. **Shilingi bilioni 3.4** kwa ajili ya kuimarisha uratibu wa utekelezaji wa Mpango Kazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto;
iii. **Shilingi bilioni 2.3** kwa ajili ya kukuza usawa wa jinsia, uwezeshaji wa wanawake kiuchumi, uhamasishaji wa teknolojia sahihi kwa wanawake wajasiriamali, uratibu wa upatikanaji wa huduma za kifedha kwa wanawake kwa kujiunga kwenye vikundi vya kiuchumi, SACCOS, VICOBA;
iv. **Shilingi bilioni 0.5** kwa ajili ya kuimarisha usimamizi na uratibu wa Mashirika yasiyo ya Kiserikali kwa kuzingatia Sheria ya Mashirika yasiyo ya Kiserikali Na.24 ya mwaka 2002 pamoja na Kanuni zake imetengewa;
v. **Shilingi billioni 0.4**Kuimarisha huduma za ustawi wa jamii kwa wazee na watoto walio katika mazingira hatarishi ikiwemo kuboresha miundombinu ya makazi;
vi. **Shilingi bilioni 0.3** Kuamsha ari ya wananchi kushiriki katika shughuli za maendeleo ikiwemo ujenzi wa makazi bora mijini na vijijini imetengewa**;** na
vii. **shilingi 0.3 bilioni** Kuimarisha upatikanaji wa haki na maendeleo ya mtoto ikiwemo utekelezaji wa afua kuhusu haki zao imetengewa;

## Habari, Michezo na Utamaduni



Katika mwaka wa fedha 2019/20 jumla ya **Shilingi billion 30.879** zimetengwa ili kutekeleza Sera, Sheria na Mipango mbalimbali ya Serikali zinazohusu Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo. Baadhi ya matumizi ni pamoja na:

i. **Shilingi bilioni 5** kwa ajili ya upanuzi wa usikivu TBC.
ii. **Shilingi bilioni 1** kwa ajili ya Habari kwa umma.

## 6.2.5 Hifadhi ya Jamii



Sekta ya hifadhi ya jamii kwa mwaka 2019/20 imetengewa jumla ya **Shilingi bilioni 1,867.08** ili kuwezesha makundi mbalimbali kushiriki kikamilifu katika shughuli za maendeleo na kijamii. Baadhi ya matumizi kwenye sekta hii ni kama ifuatavyo:

i. **Shilingi bilioni 19.93** kwa ajili ya upatikanaji wa huduma za msingi kwa Wazee wasiojiweza na Watoto walio katika mazingira hatarishi;
ii. **Shilingi bilioni 1,617.62** kwa ajili ya Mifuko ya Hifadhi ya Jamii; na
iii. **Shilingi bilioni 229.52** kwa ajili ya Mfuko wa bima ya afya.

## 6.2.6 Ulinzi, Utii wa Sheria na Usalama



Katika mwaka wa fedha 2019/20 jumla ya Shilingi **bilioni 2,965.98** kwa ajili ya kuimarisha ulinzi, usalama na masuala ya utoaji wa Haki. Shughuli zitakazotekelezwa ni pamoja na ununuzi wa zana na mitambo ya Jeshi, operation maalum, kukabiliana na majanga, uthibiti wa uhamiaji na upatikanaji wa haki kwa wakati. Baadhi ya maeneo yaliyopewa kipaumbele ni pamoja na:

i. **Shilingi bilioni 133.90** kwa ajili ya operesheni maalum za kukabiliana na majanga, uhalifu na uthibiti wa uhamiaji ndani ya nchi;
ii. **Shilingi bilioni 128.00** kwa ajili ya Ununuzi wa Zana na Mitambo ya Jeshi, Ujenzi na Ukarabati wa Makambi ya Jeshi ili kuyaimarisha Majeshi ya Ulinzi kwa vitendea kazi na mazingira ya kazi kwa ujumla;
iii. **Shilingi bilioni 80.07** kwa ajili ya kusimamia upatikanaji wa Haki Mahakamani, Mabaraza ya Usuluhishi pamoja na mashauri yote yanayohusu haki za binadamu na za kikatiba; na kupambana na utumiaji na usafirishaji wa dawa za kulevya;
iv. **Shilingi bilioni 14.01** zimetengwa kwa ajili ya Ujenzi na Ukarabati wa Majengo ya Mahakama Kuu, Mahakama za Wilaya na Mahakama za Mwanzo nchini;
v. **Shilingi bilioni 10.00** kwa ajili ya Uendelezaji wa Shughuli za Utoaji wa Vitambulisho vya Taifa;
vi. **Shilingi bilioni 5.00** kwa ajili ya Uendelezaji wa Mashamba na uanzishwaji wa viwanda vitakavyomilikiwa na Jeshi la Magereza;
vii. **Shilingi bilioni 4.50** kwa ajili ya Uimarishaji wa huduma za uokozi na kuzima moto wakati wa majanga mbalimbali yanapojitokeza;
viii. **Shilingi bilioni 2.00** kwa ajili ya Ujenzi na ukarabati wa nyumba za Askari Polisi na Ofisi katika Mikoa ya Kagera, Mbeya, Simiyu na Zanzibar;

### 6.2.7 Huduma za Utawala

Jumla ya Shilingi **bilioni 12,400** zimetengwa kwa mwaka 2019/20 kwa ajili ya kugharamia uendeshaji wa shughuli za Serikali zinazohusiana na Mihimili ya Serikali Kuu na Bunge, Huduma za Fedha na Bajeti, Mambo ya Nje pamoja na ugharamiaji wa Deni la Serikali. Baadhi ya matumizi kwenye sekta hii ni kama ifuatavyo:

i. **Shilingi bilioni 7,800.0** kwa ajili ya ulipaji wa Deni la Serikali;
ii. **Shilingi bilioni 2,200.0** kwa ajili ya kugharamia wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii-TASAF, Mradi wa Usimamizi wa Matumizi ya Taifa, Mradi wa Ukarabati wa Nyumba za Serikali, Mradi wa Taasisi ya Uongozi, na Mradi wa Maboresho ya Sekta ya Umma Awamu ya Tatu;
iii. **Shilingi bilioni 2,200.0** kwa ajili ya kujenga uwezo kuhusu: Usimamizi na utekelezaji wa bajeti; Mkakati wa kuongeza ukusanyaji wa mapato; Kuimarisha Mfumo wa Kodi; Kujenga uwezo wa kitaasisi kuhusu Utawala Bora; na Ujenzi na ukarabati wa jengo la ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali;
iv. **Shilingi bilioni 166.8** kwa ajili ya kugharamia huduma zinazohusiana na uendeshaji wa ofisi za balozi nje ya nchi, masuala ya kidiplomasia pamoja na mradi wa ununuzi, upanuzi na ukarabati wa majengo ya balozi za nje.

## *Orodha ya 1 Muhtasari wa mgawanyo wa Bajeti Kisekta*

| Sekta | | Bajeti ya 2019/20 (bilioni) | Asilimia |
|---|---|---|---|
| **Elimu** | | 4,511.79 | 13.63 |
| **Afya** | | 1,822.48 | 5.51 |
| **Maendeleo ya Uchumi** | Ujenzi, Usafirishaji na Mawasiliano | 5,519.48 | 16.67 |
| | Kilimo | 543.95 | 1.64 |
| | Viwanda na Biashara | 287.96 | 0.87 |
| | Nishati | 2,142.77 | 6.47 |
| | Madini | 49.43 | 0.15 |
| | Maliasili, Utalii na Mazingira | 111.32 | 0.34 |
| | Vijana, Ajira na Uendelezaji wa Ujuzi | 32.67 | 0.10 |
| **Maji, Nyumba na Maendeleo ya Jamii** | Maji | 661.09 | 2.00 |
| | Ardhi, Nyumba na Makazi | 68.18 | 0.21 |
| | Maendeleo ya Jamii | 47.01 | 0.14 |
| | Habari, Michezo na Utamaduni | 30.88 | 0.09 |
| **Hifadhi ya Jamii** | | 1,867.08 | 5.64 |
| **Ulinzi, Utii wa Sheria na Usalama** | | 2,960.98 | 8.94 |
| **Huduma za Utawala** | Huduma za Utawala (bila deni la Serikali) | 4,585.77 | 13.85 |
| | Deni la Serikali | 7,862.58 | 23.75 |
| **Jumla** | | **33,105.41** | **100.00** |

## NYARAKA REJEA ZA BAJETI

Ifuatayo ni orodha ya nyaraka zinazochapishwa na Serikali na kutumika kama chanzo cha taarifa za kuandaa bajeti:

- Dira ya Maendeleo ya Tanzania, 2025 pamoja na Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano;
- Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi 2015 – 2020;
- Mfumo wa Sera za Uchumi Jumla: Unatoa taarifa juu ya sera za bajeti na maboresho;
- Randama za Mipango ya Muda wa Kati na Mfumo wa Matumizi wa Muda wa Kati ya mwaka 2019/20;
- Mwongozo wa Mipango na Bajeti 2019/20
- Hotuba za Bajeti za Wizara za mwaka wa fedha 2019/20;
- Hotuba ya Hali ya Uchumi ya mwaka wa fedha 2019/20;
- Hotuba ya Bajeti ya Serikali ya mwaka wa fedha 2019/20;
- Sheria ya Fedha ya Mwaka 2019;
- Sheria ya Matumizi ya mwaka 2019;
- Sheria ya Bajeti 2015
- Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2019/20 (Juzuu Na. I – hadi IV).
- Sheria ya Bajeti ya mwaka 2015

Ili kupata baadhi ya nyaraka hizi na matoleo ya nyuma ya vijitabu vya Bajeti Toleo la Mwananchi, uneweza kutembelea mitandao ya:

  - Wizara ya Fedha na Mipango (www.mof.go.tz)
  - Policy Forum (www.policyforum.or.tz)

# Je, Utafanya nini na Taarifa hii?

Bajeti ya taifa ni taswira muhimu ya sura halisi ya kile ambacho Serikali inapanga kufanya kwa mwaka husika. Ukitaka kujua fedha yako ya kodi inakoenda, kama vile mpango wa kuboresha elimu, afya, n.k katika eneo lako, unaweza kuangalia namna na jinsi ambavyo mgawanyo wa fedha unafanyika, hususan kwa ajili ya maendeleo. Kijitabu hiki kinajaribu kutoa muhtasari wa baadhi ya taarifa hizi kwa namna iliyo rahisi kadiri iwezekanavyo. Hata hivyo unaweza kupata taarifa zaidi kuhusu mchakato wa uandaaji wa bajeti kutoka katika vyanzo vifuatavyo:

- Nyaraka zenye taarifa za bajeti ya Tanzania (***angalia orodha ya nyaraka za rejea***) na hasa, vitabu vinne vya Bajeti ya Serikali ambavyo vinapatikana katika Wizara ya Fedha na Mipango (yaani Juzuu Na. I hadi IV).
- Wizara ya Fedha na Mipango S.L.P 2802, Dodoma (tovuti http://www.mof.go.tz)
- Ofisi za Halmashauri na/au Maofisa katika eneo lako kama Mwenyekiti, Mtendaji wa Kijiji au
- Policy Forum, S.L.P. 38486, Dar es Salaam.

Kumbuka kwamba ni haki yako kujua bajeti hii na taarifa nyingine zinazohusiana na bajeti ya Serikali. Ongea na Viongozi wako kuhusu taarifa hizi na washirikishe watu wengine katika jamii unayoishi nayo.

……..……… (**Kwa maoni zaidi kata ukurasa huu**) ………………….

Je, una mawazo gani, maswali, hisia (unafikiria nini), au una maoni gani kuhusu bajeti ya mwaka 2019/20?

---------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------
---------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------
---------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------
---------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------

Je, unahitaji taarifa zaidi ya hii iliyotolewa katika kijitabu hiki?

□NDIYO □HAPANA

Kama ndiyo Je, unahitaji taarifa ya aina gani?

---------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------
---------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------
---------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------

Je kuna kitu kingine zaidi ambacho ungehitaji kukijua kuhusiana na bajeti?

---------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------
---------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------
---------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------
---------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------

Je, ni kwa kiasi gani kijitabu hiki kimekusaidia?

□ kiasi kikubwa □ Wastani □ Hakikunisaidia

Je kijitabu hiki kilikuwa rahisi kusoma na kueleweka?

□ rahisi sana □ Wastani □ Ngumu

Tuma au fikisha sehemu hii

**Wizara ya Fedha na Mipango-Idara ya Bajeti ya Serikali,**
**Jengo la Treasury Square,**
**18 Barabara ya Jakaya Kikwete**
**40468 Dodoma,**
**Sanduku la Barua 2802,**
**DODOMA-TANZANIA**

Au tuma kwa njia ya barua pepe kwa:
**ps@mof.go.tz**